



## BODI YA KAHAWA TANZANIA

### TANGAZO

#### UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2019/2020

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania anapenda kuwatangazia ufunguzi wa msimu mpya wa ununuzi wa kahawa kwa mwaka 2019/2020. Tangazo hili linatolewa kwa mujibu wa kanuni ya 23 (1) (2) ya kanuni za kahawa 2013. Tarehe za ufunguzi wa msimu wa kuanza kwa ununuzi wa kahawa katika kanda za uzalishaji kahawa ni kama ifuatavyo;

Na.	Kanda	Mkoa	Tarehe ya Ufunguzi
1.	Kaskazini	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 Julai, 2019
2.	Mbeya, Songwe	Mbeya, Songwe, Katavi	1 Juni, 2019
3.	Kigoma	Kigoma	1 Mei, 2019
4.	Mara	Mara, Mwanza	1 Juni, 2019
5.	Kagera	Kagera	1 Juni, 2019
6.	Ruvuma	Ruvuma, Iringa, Njombe	1 Julai, 2019

#### Mambo muhimu ya kuzingatia katika msimu huu 2019/2020:

1. Katika msimu huu mpya Bodi ya Kahawa itaanzisha utaratibu mpya wa kuendesha minada katika kanda za uzalishaji kahawa, ambapo minada ya kahawa ya kanda itafanyika katika maeneo yafuatayo:
  - **Bukoba:** Kwa ajili ya Mikoa ya Kagera, Mara, Kigoma na Mwanza
  - **Mbozi :** Kwa ajili ya Mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa na Katavi
  - **Mbinga:** Kwa ajili ya Mikoa ya Ruvuma na Njombe

Minada ya kanda itakuwa ni ya kahawa safi na itafanyika kwa mujibu wa kanuni na taratibu za uendeshaji ya minada ya kahawa zilizopo.

Mnada wa kitaifa unaofanyika Moshi utaendelea kufanyika kwa taratibu zilizipo na vyama vya ushirika vitakuwa huru kuchagua soko wanaloliona lina tija kwa kuuza kahawa ya wanachama wao.

2. Katika msimu huu utaratibu wa soko la moja kwa moja (Direct Export) umeboreshwa ambapo makampuni yanayotaka kununua kahawa ya Tanzania yanatakiwa kuwasilisha mahitaji yao ya kununua kahawa ya Tanzania na pia kununua kahawa kutoka kwa chama chochote cha ushirika (Intention to purchase coffee). Wanunuzi hao wataingia makubaliano na vyama hivyo vya ushirika baada ya kukubaliana bei kwa aina hiyo ya kahawa. Makubaliano ya bei yatasimamiwa na kamati maalum itakayoundwa na Serikali. Kahawa za madaraja yote zitaruhusiwa kuuzwa katika soko hili baada ya makubaliano kufikiwa na Bodi ya Kahawa itatoa tangazo la kuwaalika wanunuzi wa kahawa kuwasilisha mahitaji yao pamoja na bei mapema iwezekanavyo.

Pia baada ya kuingia makubaliano wanunuzi hao wataruhusiwa kuviwezesha vyama husika malipo ya awali, gharama za *certification*, usimamizi wa CPU na huduma nyingine za kuiwezesha kahawa kupelekwa sokoni kama magunia, usafiri, ukoboaji.

3. Maombi ya leseni zote mpya yatafanyika kwa kutumia mtandao katika mfumo wa ATMIS kwa kufuata *link* ya <https://atmis.kilimo.go.tz>
4. Vyama vya ushirika vinatakiwa kuanza kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima mara tu inapokuwa tayari na kuipeleka kwenye viwanda vya kukobolea kahawa ili kuharakisha zoezi la uuzaji wa kahawa za Wakulima;
5. Vyama vya msingi vitakavyouza kahawa mnadani vitaomba vibali kwa kujaza fomu Na. TCB/FG/001 zinazopatikana kwenye ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa na watasaidiwa kuomba vibali katika mfumo wa ATMIS na maofisa waliopo kwenye ofisi za kanda.
6. Vyama vya ushirika vikamilishe mapema taratibu za upatikanaji wa mitaji ili vianze ukusanyaji wa kahawa ya wakulima wao mara tu inapokuwa tayari.
7. Bodi ya Kahawa itaaza mara moja kuendesha minada ya kahawa pindi kiasi cha kutosha (stocks) zitakapokuwa tayari.
8. Halmashauri za wilaya zihakikishe kuwa CPU zote zilizoko katika maeneo yao zinatumika na zinafunguliwa mara tu kahawa inapokuwa tayari ili kufanikisha lengo la Serikali la kuongeza ubora wa kahawa na bei ya mkulima.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Bodi ya Kahawa Tanzania**  
**S.L.P. 732 – Moshi**  
**Simu: 027-27-52324**  
**Nukushi: 027-27-52026**  
**Barua pepe: [info@coffeeboard.or.tz](mailto:info@coffeeboard.or.tz)**  
**Tovuti: [www.coffeeboard.or.tz](http://www.coffeeboard.or.tz)**

# TANZANIA COFFEE BOARD



## PUBLIC ANNOUNCEMENT

### COMMENCEMENT OF THE NEW COFFEE SEASON 2019/2020

The Director General of the Tanzania Coffee Board is pleased to announce the commencing of the new coffee buying season 2019/2020. This announcement is released as per Regulation 23 (1) (2) of Coffee Regulations 2013. The dates of commencing of coffee buying season in different coffee production zone are as follows:

No.	Zone	Region	Date of commencement
1.	North	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 <sup>st</sup> July, 2019
2.	Mbeya, Songwe	Mbeya, Songwe, Katavi	1 <sup>st</sup> June, 2019
3.	Kigoma	Kigoma	1 <sup>st</sup> May, 2019
4.	Mara	Mara, Mwanza	1 <sup>st</sup> June, 2019
5.	Kagera	Kagera	1 <sup>st</sup> June, 2019
6.	Ruvuma	Ruvuma, Iringa, Njombe	1 <sup>st</sup> July, 2019

#### Issues to take cognizance of in the new season 2019/2020:

1. In this new season, the Coffee Board will begin conducting coffee auctions in the coffee production Zones. The zonal coffee auctions will be conducted in the following areas:
  - **Bukoba:** For Kagera, Mara, Kigoma and Mwanza Regions.
  - **Mbozi :** For Songwe, Mbeya, Iringa and Katavi Regions.
  - **Mbinga:** For Ruvuma and Njombe Regions.

Zonal auctions will be of clean coffee and will be conducted as per available rules and regulations of conducting coffee auctions.

The National coffee auction which is conducted in Moshi will continue to operate as per available arrangements; farmers through their Cooperatives Unions will be free to choose the market in which they find to be more profitable to sell their coffee.

2. In this season the Direct Export market window has been improved. Companies interested in buying Tanzanian coffee will be required to submit an Intent to Purchase any amount of Tanzania coffee or to buy coffee from any Cooperative Society/AMCOS. These buyers will enter into agreement with these Cooperative Societies after agreeing on a price for that type of coffee. The agreement on price will be under the supervision of a special committee of the Government. Coffee of all grades will be allowed to be sold in this market window after the agreement has been reached and the Board will promptly invite buyers to submit their intent to purchase coffee, the amount of coffee they want to buy and the price they are offering.

After entering into agreement, buyers will be allowed to support the respective Cooperative/AMCOS on first payments, cost of *certification*, supervision of CPU and other services which will facilitate coffee to be taken to the market like bags, transport, and milling.

3. Requests for all new licences will be done online through the ATMIS system by following the link <https://atmis.kilimo.go.tz>
4. All Cooperative Societies are required to collect coffee from farmers as soon as the coffee is ready and take it to the secondary processing factories in order to hasten the process of selling farmers coffees.
5. All Primary Societies which will be selling coffee directly to the auction will request the permit to sell coffee by filling form No. TCB/FG/001 available on TCB zonal offices and will be assisted to request for permits through the ATMIS system by TCB officials available in the zonal offices.
6. Cooperatives/ AMCOS should make sure they finalize the processes of obtaining working capital to ensure timely start up coffee collections from farmers as soon as it ready to be collected.
7. The Board will start conducting coffee auctions as soon as there are enough coffee stocks available.
8. District Councils should make sure all CPUs in their localities are working and start operating as soon as coffee is ready in order to meet the Government objectives of increasing the coffee quality and price of the farmer.

**Acting Director General**  
**Tanzania Coffee Board**  
**P. O. Box 732 – Moshi**  
**Telephone: 027-27-52324**  
**FAX: 027-27-52026**  
**Email: [info@coffeeboard.or.tz](mailto:info@coffeeboard.or.tz)**  
**Website: [www.coffeeboard.or.tz](http://www.coffeeboard.or.tz)**